BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Tano – Tarehe 11 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2026/2027.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

424. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa athari za madawa ya kulevya zimekuwa kubwa na zinaharibu afya za wototo wetu.

Je, kuna mustakabali gani wa watoto wetu kuwakinga na madawa ya kulevya.

**Ofisi ya Rais Ikulu:**

207. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:

Katika kujenga taswira nzuri na njema ya viongozi wetu wa kitaifa, ni kutoa huduma nzuri za makaazi pamoja na maeneo ya kufanyia kazi.

(a) Ni upi mpango wa Serikali katika kuboresha makaazi ya viongozi wa kitaifa katika kisiwa cha Pemba.

(b) Je, Mradi wa Ujenzi na Maboresho ya Ikulu ya Tibirinzi Pemba umegharimu kiasi gani cha fedha.

(c) Kwa nini Serikali imeamua kuziuza nyumba za viongozi katika eneo la Mazizini Unguja.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

88. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Kwa kuzingatia zuwio la maegesho ya vyombo vya moto katika barabara ya Michenzani kutokea mzunguko (round about) kuelekea Mlandege;

(a) Je, kwa kiasi gani zuwio hilo linawaumiza wafanyabiashara wa maeneo hayo.

(b) Ni ipi tathmini ya Serikali juu ya zuwio hilo la maegesho katika kuleta adha na usumbufu kwa wanaofuata huduma katika maeneo hayo kwa kushindwa kupakia bidhaa wanazozinunua katika eneo hilo.

(c) Kwa kuwa baadhi ya maeneo yaliyowekwa zuwio la magesho yapo mkabala na sehemu ya makaazi ya wananchi ambao wanalazimika kulaza vyombo vyao hapo kwa

usalama zaidi, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili.

<u>**Wizara ya Fedha na Mipango:**</u>

238. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatakiwa kurudisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa wafanyabiashara wanaonunua bidhaa kutoka Tanzania bara kuja Zanzibar. Mfanyabiashara amekuwa akidai kodi hiyo anapofaili ritani, na kutakiwa kurudishiwa bakaa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Hata hivyo, ZRA inawazuia wafanyabiashara kudai kodi hiyo yote kwa kipindi kimoja na hutakiwa baadhi kudai katika vipindi vyengine vya kufaili ritani.

(a) Je ni muongozo gani unaowataka ZRA kuwazuia wafanyabiashara kutotumia kodi hiyo yote kwa pamoja katika malipo yao ya kodi ya marejesho ya mauzo.

(b) Ni lini ZRA itarahisisha utaratibu wa kurudisha bakaa ya kodi hiyo kwa njia ya cash, ili kuongeza wigo wa ulipaji kodi bila ya shuruti.

(c) Je, tofauti ya asilimia tatu (3%) baina ya VAT ya ZRA na TRA, kwanini hairudishwi, inabakia TRA.

349. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipago:

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ni miongoni mwa Mifuko muhimu sana ya kuwahudumia wananchi baada ya kustaafu, ambapo pamoja na mambo mengine, miongoni mwa faida wanazotakiwa kuzipata wachangiaji wa Mfuko huo, ni fao la matibabu.

Je, ni wananchi wangapi wamefaidika na fao la matibabu kupitia Mfuko wa ZSSF.

466. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Moja kati ya njia zinazoleta uhuru na uhalali wa kiushindani wa kibiashara katika kumpata mzabuni, ni kutumia njia ya ushindani wa wazi *(Open Competitive Bidding)*

(a) Ni miradi mingapi mikubwa ya kimkakati ambayo Serikali imewapata wazabuni pasi na kutumia njia hiyo.

(b) Ni hatua zipi ambazo Serikali imezichukua kwa mawizara, mashirika na taasisi zake ambazo utekelezaji wa miradi yake haitumii njia ya ushindani wa wazi wakati wa kumpata mzabuni.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

26. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwepo na ongezeko la ajali za barabarani, hususani zinazohusisha usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda, ambazo zinaendelea kusababisha vifo, majeraha makubwa na ulemavu wa kudumu.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu wa kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani, hususani zinazosababishwa na usafiri wa bodaboda.

432. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa ujenzi wa barabara kuu za ndani katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Je, kuna mpango gani ya kuwajengea barabara wananchi wa Kwale-Gongo, ili kuepukana na tatizo linalowakabili.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

105. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Katika Wilaya ya Micheweni kuna mwananchi mzalendo amejenga kituo kizuri cha Kulea Watoto Yatima na kituo hicho amekiwekea mradi wa Kituo cha Mafuta, ili kukihudumia miaka yote. Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Ustawi wa Jamii ilimshauri mwanachi huyo kuongeza eneo mkabala na kituo hicho na yupo tayari endapo atapewa eneo hilo.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara, itamsaidia vipi mwananchi huyu kupatiwa eneo hili, ili kutanua huduma za kituo hicho cha watoto yatima.

(b) Kwa kuwa mwananchi huyu yupo tayari kwa gharama zake kuliendeleza eneo hilo atakapopatiwa, ni lini Serikali itaharakisha kumpatia eneo hilo, ili aweze kusaidia kuwahudumia mayatima hao.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

170. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kuanzishwa kwa Taasisi ya Ubora wa Viwango Zanzibar (ZBS), kulikuwa na lengo la kutoa msaada kwa jamii ya Zanzibar, katika kudhibiti ubora wa vifaa pamoja na vyakula vinavyoingia na kutumika nchini kutoka nje. Hivi sasa, taasisi hiyo inaonekana kukosa muendelezo mzuri kwenye majukumu yake, hasa kwenye udhibiti wa ubora wa vitu ama vifaa vinavyoingia Zanzibar.

(a) Hadi sasa, ZBS imejikita vipi kwenye kufanya operation za kuzuia bidhaa zilizoingia sokoni bila ya kukaguliwa.

(b) Kwanini ZBS haitumii mfumo wa ‘inspection from origin country’ kwa waingizaji wote wa mizigo kutoka nje kama wenzetu Tanzania Bara.

(c) Ni lini Serikali itatoa ripoti ya kina kwa wananchi wa Zanzibar, juu ya hali ya ubora wa matumizi ya vifaa vinavyoingia nchini.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

301. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kuwa kuna uvamizi mkubwa wa ardhi kwa wakaazi wa shehia za Ndagoni na viunga vyake, huku kukiwa na malalamiko kwamba baadhi ya viongozi wa shehia wanashiriki katika vitendo hivyo bila ya kushirikishwa wananchi wanaotumia maeneo hayo kwa shughuli zao za maisha zaidi ya miaka mia moja sasa.

(a) Je, Serikali inautambua vipi mvutano huo unaozidi siku hadi siku.

(b) Je, Serikali inawapa matumaini gani wananchi hao kabla ya kuzuka kwa mgogoro ili kuepusha maafa.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

242. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

Miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGaz) imezitaka taasisi zote za Serikali kuhifadhi na kupatikana tovuti zao katika miundombinu ya eGaz, kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuboresha usalama wa mtandao na mifumo ya Serikali. Hata hivyo, tovuti nyingi zimekuwa zinasuasua upatikanaji wake lakini pia zikipoteza *data* chini ya uhifadhi wa eGaz.

(a) Kwa nini eGaz imekuwa ikikumbana na changamoto za upotevu wa taarifa za tovuti inazozihifadhi mara kwa mara.

(b) Kwa nini eGaz imeshindwa kuwa na *backup* madhubuti ya kuhifadhi taarifa za tovuti ili kusaidia kuokoa taarifa wakati wa khitilafu.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasilisili na Mifugo:**

453. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar ni kisiwa ambacho hakina ardhi ya kutosha kwenye uzalishaji wa chakula.

Ni hatua zipi zilizochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

480. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Mtemani Sekondari inao upungufu mkubwa wa madarasa ya kusomea, jambo linalopelekea kuazima madarasa ya skuli ya msingi Mtemani.

(a) Je, Serikali inautambua vipi upungufu huo.

(b) Ni lini hasa tatizo hili litaondolewa.

## Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

367. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza vipaji na ujuzi wa vijana katika jimbo la Uzini.

## Wizara ya Afya:

303. MHESHIMIWA MIHAYO JUMA SULEIMAN (Jimbo la Mwera) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Kianga kilichojengwa kupitia mradi wa TASAF kinahudumia shehia ya Kianga, Dole na Mwera pamoja na shehia za jirani katika maeneo ya Mwera Mwembemchomeke, Masingini na Kizimbani ambapo inafika kuhudumia zaidi ya wagonjwa 2500 kwa mwezi.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuboresha majengo pamoja na kujengwa kituo kipya kitakachoweza kutoa huduma bora.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

376. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,Utumishi na Utawala Bora:

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea walimu kutokupimwa utendaji wao wa kazi kila mwaka, kinyume na Muongozo uliotolewa na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, hali inayopelekea kutopandishwa cheo kwa kipindi kirefu.

(b) Kwa nini Serikali haioni haja ya kuanzisha mfumo mpya wa Upimaji Utendaji Kazi na kuondokana na Mfumo wa Tathmini ya Utendaji wa Kazi Ulio Wazi (OPRAS).

(c) Ni upi Mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa suala la upimaji utendaji kazi linakuwa ni endelevu na linatekelezwa na taasisi zote za umma, ili kuongeza uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa umma.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,
11 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR